



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

+255 24 223 1095
S. L. P 3681



7 Barabara ya Gymkhana, 71102 Mjini Magharibi
Kikwajuni - Zanzibar



info@trosmz.go.tz



www.trosmz.go.tz



BA.82/120/01/01/01

08/04/2024.

Watendaji Wakuu,
Taasisi za Uwekezaji wa Umma,
ZANZIBAR

WARAKA WA MSAJILI WA HAZINA NAMBA 1/2024

KUH: MAREKEBISHO NA MAPITIO YA SHERIA NA KATIBA ZA TAASISI ZA UWEKEZAJI WA UMMA

Kwa hesima naomba uhusike na mada hapo juu.

1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Msajili wa Hazina imebaini kuwepo kwa Sheria nyingi za uanzishwaji wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma pamoja na Katiba (MEMART) ambazo zimeshapitwa na wakati hivyo haziendani na shughuli za sasa za Taasisi hizo au haziendani na kuwepo kwa Sheria mpya mbali mbali zilizoanzishwa hivi karibuni ikiwemo **Sheria Namb. 6 ya mwaka 2021** ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Changamoto hii inasababisha kuwepo kwa ugumu katika jukumu la usimamizi na kushajihisha maendeleo ya Taasisi husika kutokana na mgongano wa sheria uliopo.

2.0 MADHUMUNI YA WARAKA

Madhumuni ya Waraka huu ni kuhakikisha kuwa Sheria pamoja na katiba zote za Taasisi za Uwekezaji wa Umma (MEMART) zinafanyiwa mapitio na marekebisho ili ziweze kuendana na vifungu mbali mbali vya Sheria zilizokuwepo sasa ikiwemo **Sheria Namb. 6 ya mwaka 2021** ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina, kupitia kifungu



+255 24 223 1095



S. L. P 3681



7 Barabara ya Gymkhana, 71102 Mjini Magharibi
Kikwajuni - Zanzibar



info@trosmz.go.tz



www.trosmz.go.tz

cha 6(g) cha Sheria Namb. 6 ya mwaka 2021 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, ambapo imepewa jukumu la kutoa miongozo mbali mbali kwa ajili ya usimamizi wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma, ina lengo la kuzitaka kila Taasisi za Uwekezaji wa Umma kuanza utaratibu kuzipitia upya na kuzifanyia marekebisho Sheria zao ili ziendane na malengo makuu ya Taasisi hizo kwa wakati wa sasa.

3.0 WANAOHUSIKA NA WARAKA HUU

Waraka huu utazihusu Taasisi zote za Uwekezaji wa Umma zinazosimamiwa chini ya Sheria Namb. 6 ya mwaka 2021 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kama ifuatavyo: -

- a) Mashirika yote ya Serikali yaliyoanzishwa kwa Sheria zao (Establishment Act); na
- b) Makampuni yote ya Serikali yaliyoanzishwa na kuendeshwa kwa Sheria ya Makampuni Namb. 15 ya mwaka 2013. Yanatakiwa kuzipitia upya MEMART zao.

4.0 UTEKELEZAJI WA WARAKA

Kwa Mashirika ya Umma, yanatakiwa kuanza utaratibu wa kuzipitia upya Sheria zao katika mwaka wa Fedha wa 2024/2025 na kuwashirikisha wadau mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kutoa maoni ya uboreshaji wa Sheria hizo. Kwa upande wa Makampuni, Bodi zinatakiwa kuanza kuzipitia Katiba (MEMART) zao na kuwasilishwa rasimu katika Ofisi ya Msajili wa Hazina katika **Robo Mwaka ya mwanzo** ya mwaka 2024/2025 (July/Septemba 2024) kwa ajili ya kutoa maoni kabla ya kupitishwa katika Mkutano Mkuu wa Wanahisa unaofuata (**Shareholder's Meeting**). Ikiwa Taasisi itaweza kurekebisha kwa haraka itakuwa vyema.



+255 24 223 1095



S. L. P 3681



7 Barabara ya Gymkhana, 71102 Mjini Magharibi

Kikwajuni - Zanzibar



info@trosmz.go.tz




www.trosmz.go.tz

5.0 KUANZA KUTUMIKA KWA WARAKA HUU

Waraka huu utaanza kutekelezwa kuanzia tarehe ya Waraka huu na pale ufafanuzi utakapo hitajika mnaelekezwa kuwasiliana na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar.

Ahsante,



**WAHEED MUHAMMAD IBRAHIM SANYA,
MSAJILI WA HAZINA.**



NAKLA;

**KATIBU WA RAIS- IKULU,
ZANZIBAR.**

**KATIBU MKUU KIONGOZI,
ZANZIBAR.**

**KATIBU MKUU,
OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO,
ZANZIBAR.**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI,
ZANZIBAR.**



+255 24 223 1095



S. L. P 3681



7 Barabara ya Gymkhana, 71102 Mjini Magharibi
Kikwajuni - Zanzibar



info@trosmz.go.tz



www.trosmz.go.tz